

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

MKOA WA DAR ES SALAAM

Anwani ya Simu:
Simu: 2203156/58
Fax: +25522203213
Tovuti: www.dsm.go.tz
Barua Pepe: ras@dsm.go.tz



OFISI YA MKUU WA MKOA
3 Barabara ya Rashidi Kawawa,
S.L.P 5429,
12880 -DAR ES SALAAM.

Tanzania

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Tarehe 12/05/2017 Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam Mhe. Paul C. Makonda alifanya ziara ya kukagua ujenzi wa wodi za kisasa za wazazi na watoto zinazoendelea kujengwa katika Wilaya tatu za Ilala – Amana Hospitali, Temeke – Temeke Hospitali na Kinondoni – Mwananyamala Hospitali.

Ujenzi huo wa majengo ya ghorofa tatu kwa kila jengo la wodi ya wazazi na watoto katika Wilaya hizo utawawezesha zaidi wakina mama 1350 na watoto wao kupata huduma za malazi wakati wa matibabu.

Wodi hizi zikikamilika zitasaidia kuondoa kero ya mlundikano kwa kina mama wajawazito na watoto wao katika Mkoa wa Dar es Salaam.

Ujenzi huu ni kwa ufadhili wa wadau wa maendeleo ya Mkoa wa Dar es Salaam.

Imetolewa Na:-

Kitengo cha Habari na Uhusiano

OFISI YA MKUU WA MKOA

DAR ES SALAAM

15/05/2017